

## **TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO YA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI**

### **1.0 MPANGO WA MAENDELEO YA ELIMU YA MSINGI (MEM)**

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ulianza mwaka 2002. Utekelezaji wake hadi Machi, 2010 ni kama ifuatavyo:

- (i) Wanafunzi wa shule za msingi walioandikishwa mwaka 2000 darasa la I –VII walikuwa 4,382,410. Kwa mwaka 2010 idadi yao imeongezeka hadi 8,786,324. Hivyo kuwa na ongezeko la wanafunzi 4,403,914, sawa na asilimia 100.5;
- (ii) Jumla ya walimu wa Daraja IIIA 86,252 wameajiriwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (iii) Jumla ya madarasa 43,221 yamejengwa na madarasa 726 ujenzi upo kwenye hatua mbalimbali za kukamilishwa;
- (iv) Jumla ya nyumba 13,752 zimejengwa katika maeneo mbalimbali na nyumba 899 zipo katika hatua mbalimbali za kukamilishwa;
- (v) Jumla ya matundu ya vyoo 37,023 yamejengwa na matundu 17,775 yapo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi;
- (vi) Madawati 645,138 yametengenezwa;
- (vii) Fedha zilizotumika kujenga miundombinu hiyo hapo juu zimetokana na fedha zilizopelekwa na Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na nguvu za wananchi;
- (viii) Jumla ya watoto 12,136,509 wameandikishwa kuanza darasa la kwanza katika kipindi hicho cha utekelezaji na jumla ya wanafunzi 69,062,191 wameandikishwa darasa la kwanza hadi la saba katika kipindi hicho;
- (ix) Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2002 hadi 2009 jumla ya wanafunzi 5,538,246 walifanya Mtihani wa Kuhitimu Elimu ya Msingi. Kati ya hao, wanafunzi 2,797,436 walifaulu na wanafunzi 2,275,507 walichaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari katika kipindi hicho;
- (x) Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ulipoanza mwaka 2002, Uwiano kwa Kitabu kwa Mwanafunzi ulikuwa wastani wa Kitabu kimoja kwa wanafunzi ishirini (1:20). Uwiano huu umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka kutokana na fedha za uendeshaji (Capitation Grant) zilizokuwa zikipelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kununulia vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia. Hadi mwaka 2009/2010, uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi umefikia wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu (1:3)

- (xi) Katika kipindi hicho, jumla ya walimu 6,578 wa Daraja la IIIB/C wamejiendeleza na kufikia kiwango cha Daraja IIIA. Aidha, walimu 1,577 wamejiendeleza na kufikia kiwango cha Stashahada.

## **2.0 Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES)**

Utekelezaji wa Mpango huu ulianza mwaka 2004. Utekelezaji wake hadi Machi, 2010 ni kama ifuatavyo:

- (i) Jumla ya wanafunzi 4,796,959 wamejiunga na kidato cha kwanza katika kipindi hicho. Kwa mwaka 2004 kulikuwa na wanafunzi 432,599 kuanzia kidato cha kwanza hadi sita. Kwa mwaka 2009, jumla ya wanafunzi 1,466,402 wameandikishwa katika kidato cha kwanza hadi sita. Hivyo kuwa na ongezeko la wanafunzi 1,033,843;
- (ii) Hadi mwaka 2009 jumla ya Wanafunzo wote walioandikishwa katika shule za sekondari wamefikia 6,010,670;
- (iii) Kati ya mwaka 2002 hadi 2009, jumla ya wanafunzi 956,109 walifanya Mtihani wa Kumaliza Kidato cha Nne. Kati yao, wanafunzi 758,529 walifaulu na wanafunzi 224,854 walichaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha tano;
- (iv) Shule za sekondari zimeongezeka kutoka shule 1,291 mwaka 2004 hadi kufikia shule 4,102 mwaka 2009.